

Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea

Episode 06 “Nawa Mikono”

Author: Njoki C. Muhoho
Medical Advisor Dr Ng’ethe Muhoho
Editor Maja Braun
Kiswaheli Eric Ponda

Scene	Characters	
1	1. SAM 2. CHEMU 3. EDITH 4. MARIA	SAM – 17, m. EDITH – 40, f. MARIA – 43, f.
2	1. SAM 2. CHEMU 3. EDITH 4. MARIA	EDDI– 36, m. DR SALLY – 34, f. CHEMU – 15, f.
3	1. SAM 2. CHEMU	GROUP OF STUDENTS – all male
4	1. SAM 2. EDDI 3. EDITH 4. CHEMU 5. NARRATOR	NARRATOR
5	6. SAM 7. CHEMU 8. EDDI 9. GROUP OF	

	STUDENTS	
	10. NARRATOR	

INTRO

MUSIC: THEME MUSIC

- 01. NARRATOR** Hujambo msikilizaji na karibu kwa sehemu ya sita ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako, tukiwa bado tunazungumzia masuala ya *USAFINA UGONJWA WA KUHARA*.Katika kipindi kilichotangulia Sam na Familia yake walijifunza kuhusu chanzo chengine cha ugonjwa wa kuhara ambacho ni Chango.Pia walishuhudia jinsi maji yanavyoweza kuchanganyika na vidudu na Vimelea vinavyosababisha ugonjwa huu.Katika Makala ya leo Familia hiyo itajifunza mbinu mbali mbali za kuhakikisha kuwa maji yanabakia salama yakiwa kwenye chanzo chake na pia wakati wa matumizi. Elimu hiyo inasambazwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa.Ungana nasi hadi mwisho upate kufahamu yanayojiri.

SCENE 1: MAMA SAM'S HOME

02. SFX: SOUNDS OF POTS AND PANS. A FIRE IS CRACKING.

- 03. MARIA** Edith, Nahisi njaa sana hata naweza kumla Farasi mzima...!

04. **EDITH** **Hapa watu hawafugi farasi rafiki yangu Maria, labda punda.**
05. **MARIA/EDITH** *(both laugh heartily)*
06. **MARIA** *(still laughing)* **Najua, lakini si unaelewa nina maana gani?. Hebu nipe hiyo nyanya. Nitaila ninaposubiri chakula chako kiive.**Kwanini chakula kinachukua muda mrefu kuwa tayari?. Sam hebu nipe nyanya moja kutoka kapuni..
07. **SAM** **Unataka iliyoiva sana au tosa kidogo.?**
08. **EDITH** **Hebu mpe tu nyanya yoyote!**
09. **CHEMU** **Lakini kwanza lazima uioshe.**
10. **MARIA** Chemu, wewe umeketi karibu na kapu hilo na wasikia nikilia njaa. Kwani kula nyanya moja ndogo kunazua mjadala wa elimu?Hebu kuwa binti mzuri na unipe nyanya hiyo.
11. **SAM** **Lazima tuioshe kwanza!. Subiri dakika moja tu!**
12. **MARIA** *(angry)* **Hebu nipe hiyo nyanya wewe msichana..!**
13. **CHEMU** Lakini lazima kwanza tuioshe!
14. **MARIA** **Ilete.... upesi..!**

15. **EDITH** (*angry*) Tafadhali mpeni hiyo nyanya!... upesi !
16. **SAM** (*calmly*) Shangazi Maria, kumbuka nilivyofanya katika shamba lako wakati nikiugua kuhara...! Bado unataka kula nyanya mbichi kabla ya kuiosha!
17. **MARIA** Ooooh hapana... hapana...! Ioshe basi... sasa unangoja nini? Osha na uifute... upesi... ioshe!. Kwani ulitaka kunipa bila kuiosha? Hehehe... vidudu na magonjwa haya yote yanayosubiri kuyavamia matumbo yetu.Unawazimu?

BRIDGE MUSIC

SCENE 2: EDITH’S HOME LATER

18. **SFX: SOUNDS OF CUTLERY AND CROCKERY.**
19. **EDITH** Sam tafadhali mpe Maria hiki chakula
20. **MARIA** (*surprised*) Oh, Mama Sam kumbe bado chakula kimesalia kwenye sufuria....?! Niongezee tafadhali. Nilishakuarifu nina njaa kweli.
21. **MARIA** Sawa Maria...! Mimi nakupenda sana kwa sababu ni mkweli.
22. **SAM** Haya hiki hapa chakula.

23. **MARIA** **Ahsante sana Sam. Ni kweli mama Sam, kwanini nife njaa kwasababu ya kuona haya? Nimekuwa nikihisi njaa mchana kutwa. Hata hivyo samahani kwa ulafi wangu maana sitawasubiri!. Nitakula mara moja kwa mikono yangu.**
24. **CHEMU/SAM** **Ngoja, ngoja kwanza!**
25. **EDITH** **Nini tena ? Enyi watoto nyi....muna nini akilini? Kwanza mlimnyima nyanya, sasa hamtaki ale chakula kwa mikono yake.. Kwanini?**
26. **SAM** **Hatakula kwa mikono yake Mama... ni vidole!**
27. **MARIA** **(very angry) Enyi watoto, niacheni nile ninavyotaka mwenyewe, tafadhali sitaki kusikia tena kelele wakati ninapofurahia chakula hiki kitamu... sawa?**
28. **SAM** **Lakini unapaswa kunawa mikono kabla ya kula.**
29. **MARIA** **Tena...?**
30. **SAM** **Ehhe ikiwa hutaki kuumwa kama mimi....!**
31. **CHEMU** **(Pleading) Tafadhali..... Mama..! hungenda kuona mambo mabaya, kama yale yaliyomfika Fatu yakitokea tena sivyo..?.Sitaki ufe!.**

- 32. EDITH** Maria,Hebu angalia jinsi kauli zako zilivyomsononesha binti yako...!.Machozi yanamlengalenga. Nawa mikono Maria.
- 33. MARIA** Kwanini? Si mimi peke yangu aliyeshika shika vitu vichafu hapa...! Hivi mna maana kuwa mimi ndio mchafu pekee hapa...?
- 34. CHEMU** La hasha mama ...! Sio kuwa wewe ni mchafu...!. Ila ni kuwa vidudu vinavyosababisha magonjwa viko kila mahali,kwenye vitu,tunaposalimiana na hata vitu tunavyoshika... Kila mahali, sivyo, Sam?
- 35. SAM** Hebu kumbuka vitu nilivyoshika au mahali nguo zangu zilipowekwa wakati nilipokuwa nikiugua ugonjwa wa kuhara?
- 36. MARIA** Nikilifikiri hilo... natamani kuihama nyumba hii na nisirudi tena!
- 37. EDITH** Sam, unajaribu kumuogofya rafiki yangu Maria?
- 38. CHEMU** La... sio kuwa namtia hofu mtu yeyote.Sisi sote tunawapenda na ingekuwa bora mukiendelea kuwa na afya nzuri.
- 39. EDITH** Hebu kuleni chakula chenu upesi kinazidi kupoa.
- 40. SAM** Chemu, lete beseni la maji na sabuni tunawe mikono.

**41. NARRATOR INAVYOONEKANA, WATU WAZIMA WANAHITAJI
MAFUNZO ZAIDI KULIKO WATOTO. SAM NA
CHEMU WALIJIFUNZA MENGI BAADA YA
UGONJWA WA KUHARA KUIVAMIA NYUMBA YA
MAMA SAM NA MWISHOWE KUKISABABISHA
KIFO CHA FATU.HATA HIVYO KUNA MENGI
YANAYOWATIA WASIWASI.....BAADA YA
CHAKULA CHA MCHANA WOTE
WALIANDAMANA KUNYOSHA MIGUU KIDOGO.**

SCENE 3: FOOT PATH

42. **SFX** **NATURAL SOUNDS. TWO PAIRS OF FEET WALKING.**

43. **CHEMU** (*raps*)

Osha mikono yako, Osha mikono yako
Mikono safi tu, hutumiwa kwa kula
Wasiojali tu, hutumia mikono michafu
Baada ya msala, Osha mikono yako
Dumisha afya yako, Osha mikono yako
Sasa sasa tunaweza kuimba pamoja, na muimbe
vizuri.

Wash your hands

Only washed hands
should be used,
to eat.

44. **SAM** (*Raps like he is reading words*)

Wash your hands
Only washed hand

45. **CHEMU** Ngoja..! ngoja.! umekosea wizani!!.

46. **SAM** Lakini maneno ameyapatia vizuri. Nitajaribu kuufuata
wizaniila sio wakati huu baadaye....

47. **CHEMU** Sitakuacha upumzike hadi utakapoweza kuimba
wimbo huu inavyotakikana.

48. **SAM** **Nakuahidi nitajifunza. Lakini kwa sasa waonaje nikipukufukuza hadi kwenye mti ule ...!**
49. **CHEMU** Sawa twende... sawa... *on your marks*... !
50. **SFX: FEET RUN OFF VERY FAST**
51. **CHEMU** Ahaa...wewe ni muongo... kuna hila..!...
52. **SFX: FOOTSTEPS STOP.**
53. **SAM** **(From a distance)** Lazima nikuonyeshe kwamba nimerejesha nnguvu zangu mwilini...! Nina hamu sana ya kushiriki kwenye mashindano yajayo shuleni!
54. **CHEMU** Natumai utaibuka mshindi.
55. **SAM** Umesema nini, eti umesemaje....! Hebu njoo hapa nikuonyeshe!
56. **CHEMU** **(giggling uncontrollably)** Wacha mzaha Sam niwache niwaaaaache.... ! Sawa basi umeshinda.. ama kwa hakika pia utashinda kwenye mashindano hayo!
57. **SAM** Sawa nimekuwacha... !
58. **CHEMU** Sawa, lakini Sam, nafikiri tunaweza kuwafunza wanafunzi wote shuleni wimbo huu.Utawakumbusha daima umuhimu wa kunawa mikono yao kila mara..
59. **SAM** Na hivyo kujiepusha kuambukizwa ugonjwa wa kuhara kama ilivyotokea kwangu!

60. **CHEMU** Kweli iwapo watakuwa na mazowea ya kunawa mikono kila mara huenda wakajiepusha na maambukizi ya ugonjwa huu pamoja na kushindwa kwenda shule kama wewe ulipokuwa mgonjwa
61. **SAM** Au kifo kama ilivyotokea kwa Mtoto Fatu.
62. **CHEMU** (*sadly*) Ni kweli lazima tuwafunze wimbo huu. Tujaribu kuzungumza na mwalimu wetu kesho.
63. **SAM** Ndio.... Sasa tushindane kukimbia hadi mwisho wa barabara.
64. **SFX RUNNING FEET – AWAY**
65. **SAM** Hapana... subiri usianze kukimbia kwanza ... si sawa....

BRIDGE MUSIC

66. **NARRATOR** **Mambo yanakwenda vizuri kati ya Sam na Chemu.** Kama mmoja aliyenusurika, Sam anaitumia fursa hiyo kuwaelimisha vijana wengine athari za ugonjwa huo wa Kuhara. Ikiwa watatumia hekma kuwahamasisha watoto wengine, mfano kupitia wimbo wao wa Rap bila shaka lengo lao litatimia.

SCENE 4: MAMASAM'S HOME

67. **EDDI** Niliwaahidi nitakuwa nikiwatembelea jamaa zangu kuwajulia hali mara kwa mara... Nimekuwa nikijihusisha zaidi na masuala ya kazi ya afya ya jamii...hata hivyo kipi kilicho muhimu zaidi kuliko afya ya jamii yako?
68. **EDITH** Ahhhh Eddi tumeshukuru sana..!.
69. **EDDI** Ehhe, Sam, sasa unaendeleaje shuleni?
70. **SAM** **Naendelea vizuri tu mjomba Eddi, lakini nilikuwa na kibarua cha kuwa sawa na wenzangu kwasababu sikuenda kwa muda.**
71. **EDDI** Umekosa kwenda shule kwa muda gani vile? Wiki mbili?
72. **CHEMU** Alikosa kuenda kwa siku 17...
73. **EDITH** Chemu, mwache mwenyewe aseme!
74. **SAM** Kama wiki tatu hizi mjomba... lakini... lakini...
75. **EDDI** Ehhe kuna nini?
76. **SAM** Kwa vile sasa nimeugua ugonjwa huu wa kuhara, najua jinsi mtu anavyoweza kuambukizwa, na nahofia wanafunzi wengi shuleni huenda wakaambukizwa kila wakati.
77. **EDDI** Kwanini unafikiria hivyo?

- 78. SAM** Kwa sababu hawanawi mikono... na vyoo vyetu ni vile...
- 79. CHEMU** Vyoo hivyo ni vichafu na wanafunzi wengi hawanawi mikono kila baada ya kuvitumia ..
- 80. EDDI** Jee naweza kuja shuleni kuzungumza nao. Hilo pia ni jukumu langu kama mhudumu wa afya ya jamii....
- 81. CHEMU** Litakuwa jambo la busara sana.
- 82. SAM** Mjomba Eddi tafadhali njoo utusaidie..

BRIDGE MUSIC

- 83 NARRATOR** WAJIBU WA KUDUMISHA USAFI SI WA FAMILIA HII PEKEE. LAZIMA WAHAKIKISHE KUWA MARAFIKI WAO PIA WANAIKUPATA ELIMU HIYO. KWA HIVYO ,KESHO YAKE,DARASANI KWA KINA SAM

SCENE 5: SECONDARY SCHOOL

84 SAM **Habari ya asubuhi wanafunzi wenzangu. Ahsante mwalimu Grace . Ahsante kwa kunipa nafasi hii kumleta mjomba wangu Eddi ili atuelimishe kuhusu masuala ya usafi.** Wanafunzi wenzangu nafurahi nawatambulisha mjomba Eddi ambaye ni afisa wa huduma za afya ya jamii..

85 ***STUDENTS: CLAPPING***

86 SAM Kadhalika nimefurahi kumtambulisha pia rafiki yangu wa dhati Chemu ambaye anasomea shule jirani ya wasichana. Wengi wetu nadhani munamfhamu

87 ***STUDENTS: CHEEKY WHISTLING***

88 EDDI Ahsante sana mwalimu Grace, mpwa wangu Sam, na rafiki yake Chemu, kwa kunialika shuleni hapa. Kama mujuavyo, Sam amekosa kuja shuleni kwa zaidi ya wiki tatu sasa. Alikuwa akihara vibaya sana Na kutokana na maradhi haya tulijifunza mengi sana. Kwanza kabisa Sam na Chemu wametunga wimbo ambao wangependa kuwafunza nyinyi pia. Ni wimbo kuhusu umuhimu wa kunawa mikono. Hebu tuwasikilize.

89 ***STUDENTS: ENTHUSIASTIC CLAPPING***

90 SAM/CHEMU (*singing beautifully*)

*Wash your hands.
Only washed hands
should be used,
to eat.
Careless people,
Don't wash their hands
after visiting the toilet.
Keep healthy.
Wash your hands.*

91 EDDI Pongezi kabisa wimbo mzuri sana. Hebu tuwapigieni makofi..

92 STUDENTS ENTHUSIASTIC CLAPPING

93 EDDI Sam na Chemu ningependa muwafunze wimbo huu wanafunzi wote hapa shuleni. Je munaweza kufanya hivyo kwa niaba yangu?

94 SAM/CHEMU Ndio mjomba Eddi..!.

95 CHEMU Mjomba Eddi lakini sisi hatuimbi tu, tuna *Rap..!!!*

96 STUDENTS CLAPPING AND WHISTLING.

97 EDDI Nimefurahi kuwaona mumechangamka. Hebu tusikilize tena.... ehh ...oohhh *Rap*. Kumbuka ni lazima tunawe mikono yetu kila tunapotoka chooni au kabla ya kula chakula. Hii ina maana tunapaswa kunawa mikono yetu mara tano kwa siku. Kila unapoimba wimbo huu unatukumbusha kunawa mikono yetu kila mara.

Sasa ***turap*** pamoja ..!

98 SAM/CHEMU/STUDENTS

*Wash your hands.
Only washed hands
should be used,
to eat.
Careless people,
Don't wash their hands
after visiting the toilet.
Keep healthy.
Wash your hands.*

BRIDGE MUSIC

OUTRO

99 NARRATOR BILA SHAKA UMUHIMU WA KUZINGATIA KANUNI ZA USAFI, SI JAMBO LA KUCHOKESHA AU LISILOSISIMUA. JAMII INAWEZA KUEPUKANA NA JANGA AU TISHIO LA KUAMBUKIZWA MARADHI IWAPO TU KILA MMOJA ATAWAJIBIKA. HADI HAPO NDIPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAKALA HAYA, NATUMAI KWAMBA UTAUNGANA NASI WAKATI MWENGINE KWA MAKALA MENGINE. UKITAKA KUSIKILIZA TENA KIPINDI HIKI AU VYENGINE VINAVYOTAYARISHWA NA DEUTSCHE WELLE AU KUTUMA MAONI YAKO UNaweza KUTEMBELEA MTANDANO WETU WA WWW.DW-WORLD.DE/LBE :HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.